

SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 53 **JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC)** JULAI 2025

WAZIRI SIMBACHAWENE AWATAKA WAJUMBE WA KAMATI ZA TSC WILAYA KUSIMAMIA WALIMU KWA WELEDI, MAADILI NA UWAJIBIKAJI



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – UTUMISHI Mhe. George Simbachawene akitoa hotuba tarehe 5 Jui, 2025 wakati wa kufunga mafunzo ya Maafisa Elimu wa Wilaya (DEO) katika ukumbi wa Chuo cha Utumishi wa Umma, Tanzania, Kampasi ya Tabora.

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz

 Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania  [tumeyautumishiwawalimutanzania](https://www.instagram.com/tumeyautumishiwawalimutanzania)

Kamati za TSC Wilaya

Zizingatie Uadilifu na Weledi

Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – UTUMISHI, Mhe. George Simbachawene aliyotoa tarehe 5 Juni 2025 mjini Tabora, imeweka wazi umuhimu wa Kamati za Ajira, Upandishwaji Vyeo na Nidhamu za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ngazi ya Wilaya katika kusimamia walimu – kundi ambalo linaunda zaidi ya asilimia 50 ya watumishi wote wa umma nchini.


Uamuzi wowote usiozingatia Sheria, Kanuni na misingi ya haki unaweza kuvuruga motisha ya walimu, kuharibu maisha ya kitaaluma na kudhoofisha mfumo wa elimu. Kamati hizi zinapaswa

kuwa mfano wa uadilifu na haki.

Mafunzo yaliyoendeshwa na Tume ni hatua muhimu, lakini utekelezaji wa yaliyofundishwa hutegemea dhamira binafsi ya kila mjumbe katika kutanguliza maslahi ya maendeleo ya Sekta ya Elimu na Taifa kwa ujumla. Wajumbe hawapaswi kuwa sehemu ya tatizo, bali suluhisho la changamoto katika utumishi wa walimu.

Kongole kwa Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kuchukua hatua muhimu ya kutoa mafunzo hayo muhimu. Imani yetu ni kuwa kila Kamati hizi zitatekeleza majumuku yake kwa weledi na ufanisi bila uonevu wowote.

KATUNI



BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti

Paulina M. Nkwama

Wajumbe

Revocatus P. Misonge
Mectildis F. Kapinga
Lameck S. Mbeya
Zachary A. Dida
Fatuma I. Muya
Edwin Mgendera

Mhariri Mkuu

Artemony T. Vincent

Mhariri

Adili J. Mhina

Msanifu Kurasa

Lucas G. Ogunde

WAZIRI SIMBACHAWENE AWATAKA WAJUMBE WA KAMATI ZA TSC WILAYA KUSIMAMIA WALIMU KWA WELEDI, MAADILI NA UWAJIBIKAJI

Na Mwandishi Wetu – Tabora.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – UTUMISHI, Mhe. George Simbachawene, ametoa wito kwa Wajumbe wa Kamati za Ajira, Upandishwaji Vyeo na Nidhamu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ngazi ya Wilaya kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa weledi, uadilifu na uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu, ili kuiwezesha sekta ya elimu nchini kuendelea kutoa matokeo chanya na ya haraka.

Wito huo umetolewa tarehe 5 Juni, 2025, wakati wa hafla ya kufunga mafunzo ya Maafisa Elimu wa Wilaya (DEOs) ambao ni wajumbe wa Kamati kutoka mikoa mbalimbali, yaliyofanyika katika ukumbi wa Chuo cha Utumishi wa Umma, Kampasi ya Tabora. Mafunzo hayo yalilenga kuwaongezea ujuzi, uelewa na uwezo wa kusimamia masuala ya maadili, ajira, na nidhamu kwa walimu wanaohudumiwa na Tume.

Katika hotuba yake, Mhe. Simbachawene alisema kuwa walimu ni kundi muhimu katika utumishi wa umma, wakiwa ni zaidi ya asilimia 50 ya watumishi wote nchini, na kwamba kazi yao ya kuandaa rasilimaliwatu yenye maarifa na ujuzi ni silaha muhimu katika mapambano dhidi ya maadui wakuu watatu wa taifa: ujinga, umaskini na maradhi.

“Walimu ni askari walioko mstari wa mbele kwenye vita ya maarifa. Kwa nafasi yao, wanahitaji jicho la karibu. Tunahitaji Kamati zetu kuhakikisha walimu wanatekeleza wajibu wao kwa heshima, kwa nidhamu, na kwa kuzingatia taratibu za utumishi wa umma,” alieleza Waziri.

Akiweka mkazo kwenye masuala ya maadili na haki, Waziri Simbachawene alisisitiza kuwa wajumbe wa Kamati hizo wanapaswa kuepuka mgongano wa maslahi, hasa wanapojihusisha na mashauri ya nidhamu ya walimu.

“Huwezi kuwa mtoa tuhuma na wakati huohuo ukawa sehemu ya



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa walimu, Prof. Masoud Hadi Muruke akitoa salamu za Tume tarehe 5 Juni, 2025 mjini Tabora wakati wa kufunga mafunzo ya Maafisa Elimu wa Wilaya (DEO) katika ukumbi wa Chuo cha Utumishi wa Umma, Tanzania, Kampasi ya Tabora.

kamati ya kusikiliza shauri la yule uliyemshitaki. Hilo ni kinyume na misingi ya haki za msingi (natural justice). Haki ya mtuhumiwa ni kupata uamuzi kutoka kwa chombo kisichoegemea upande wowote,” alionya.

Katika hatua nyingine, Waziri aliipongeza Tume kwa kuendelea kuwajengea uwezo watumishi wake pamoja na wajumbe wa Tume ngazi ya Taifa na Wilaya kupitia mafunzo ya kitaalamu yanayozingatia changamoto halisi zinazojitokeza katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Masoud Hadi Muruke, alieleza kuwa mafunzo hayo ya siku tatu yameandaliwa kwa kuzingatia mabadiliko na mahitaji ya sasa katika uendeshaji wa mashauri ya nidhamu na utekelezaji wa Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa walimu wapya.

“Mafunzo haya ni mwendelezo wa mafunzo ya awali yaliyotolewa Septemba 2024 kwa wenyevidi na wajumbe wawili wa kila Kamati ya Wilaya. Sasa tumeweza kuwafikia wajumbe wanne kati ya watano

kwa kila Wilaya, sawa na asilimia 80, na tumewakamilisha pia makatibu wa Kamati katika Wilaya zote 139 Tanzania Bara,” alisema Prof. Muruke.

Aliongeza kuwa uamuzi wa kuendesha mafunzo hayo ulitokana na changamoto zilizojitokeza, ikiwa ni pamoja na ucheleweshaji wa mashauri ya nidhamu, ukiukwaji wa taratibu, pamoja na mashauri kurejeshwa kwa ajili ya kuanza upya hali ambayo ilisababisha ucheleweshwaji wa haki na hasara kwa Serikali.

“Ni matarajio ya Tume kuwa kupitia mafunzo haya, tutakuwa tumewapa nyenzo sahihi za kuendesha mashauri kwa haki, uwazi, usawa na kwa kuzingatia weledi. Tumeazimia kuwa na mfumo wa nidhamu unaozingatia tija na unaomlinda mtumishi mwadilifu,” alifafanua Prof. Muruke.

Naye Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama, alieleza kuwa Tume itaendelea kuweka msukumo mkubwa kwenye kuongeza uwezo kwa ngazi zote za utekelezaji nchini, hasa kwa Kamati za Wilaya ambazo ndizo zinazokaa karibu na walimu kwa kila siku.

WAZIRI SIMBACHAWENE AWATAKA WAJUMBE WA KAMATI ZA TSC WILAYA KUSIMAMIA WALIMU KWA WELEDI, MAADILI NA UWAJIBIKAJI



Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Tabora ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Sikonge, Mhe. Cornel Lucas Magembe akitoa salamu za Mkoa tarehe 5 Juni, 2025 mjini Tabora wakati wa kufunga mafunzo ya Maafisa Elimu wa Wilaya (DEO) katika ukumbi wa Chuo cha Utumishi wa Umma, Tanzania, Kampasi ya Tabora.



Baadhi ya washiriki wa Mafunzo kwa Wajumbe wa Kamati za Ajira, Upandishwaji vyeo na Nidhamu wa Tume ya Utumishi wa Walimu ngazi Wilaya nchini wakifuatilia hotuba ya mgeni rasmi wa wakati wa kufunga mafunzo yao katika ukumbi wa Chuo cha Utumishi wa Umma, Tanzania, Kampasi ya Tabora.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Utumishi Mhe George Simbachawene (kulia) akisamiliiana na Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Utawala na Rasimaliwatu kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu tarehe 5 Juni, 2025 alipowasili mkoani Tabora kwa ajili ya kufunga mafunzo ya Maafisa Elimu wa Wilaya (DEO) katika ukumbi wa Chuo cha Utumishi wa Umma, Tanzania, Kampasi ya Tabora.

WAZIRI SIMBACHAWENE AWATAKA WAJUMBE WA KAMATI ZA TSC WILAYA KUSIMAMIA WALIMU KWA WELEDI, MAADILI NA UWAJIBIKAJI



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Mwl. Paulina Nkwama akitoa maelezo mafupi tarehe 5 Juni, 2025 mjini Tabora kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Utumishi, Mhe. George Simbachawene (katikati aliyekaa) wakati alipowasili kwa ajili ya kufunga mafunzo ya Maafisa Elimu wa Wilaya (DEO) katika ukumbi wa Chuo cha Utumishi wa Umma, Tanzania, Kampasi ya Tabora.



Mkuu wa Mkoa wa Tabora Mhe. Paul Chacha (kulia) akibadilishana mawazo ofisini kwake na Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa walimu, Prof. Masoud Hadi Muruke (katikati) na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (kushoto) kabla ya hafla fupi ya kufunga mafunzo ya Maafisa Elimu wa Wilaya (DEO) katika ukumbi wa Chuo cha Utumishi wa Umma, Tanzania, Kampasi ya Tabora.



Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Tabora ambaye pia ni Mkuu wa wilaya ya Sikonge, Mhe. Cornel Lucas Magembe akitoa salamu za Mkoa tarehe 5 Juni, 2025 mjini Tabora wakati wa kufunga mafunzo ya Maafisa Elimu wa Wilaya katika ukumbi wa Chuo cha Utumishi wa Umma, Tanzania, Kampasi ya Tabora.



Mkuu wa Chuo na Mtendaji Mkuu wa Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania, Dkt. Ernest Mabonesho akitoa maelezo mafupi tarehe 5 Juni, 2025 mjini Tabora kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Utumishi Mhe. George Simbachawene (katikati aliyekaa) wakati alipowasili kwa ajili ya kufunga mafunzo ya Maafisa Elimu wa Wilaya katika ukumbi wa Chuo cha Utumishi wa Umma, Tanzania, Kampasi ya Tabora.

WAZIRI SIMBACHAWENE AWATAKA WAJUMBE WA KAMATI ZA TSC WILAYA KUSIMAMIA WALIMU KWA WELEDI, MAADILI NA UWAJIBIKAJI



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Utumishi, Mhe. George Simbachawene (kulia) akisimamia na Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Tabora ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Sikonge Mkuu wa wilaya ya Sikonge, Mhe. Cornel Lucas Magembe tarehe 5 Juni, 2025 alipowasili mkoani Tabora kwa ajili ya kufunga mafunzo ya Maafisa Elimu wa Wilaya katika ukumbi wa Chuo cha Utumishi wa Umma, Tanzania, Kampasi ya Tabora.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Utumishi, Mhe. George Simbachawene (kulia) akisimamia na Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa walimu, Prof. Masoud Hadi Muruke tarehe 5 Juni, 2025 alipowasili mkoani Tabora kwa ajili ya kufunga mafunzo ya Maafisa Elimu wa Wilaya katika ukumbi wa Chuo cha Utumishi wa Umma, Tanzania, Kampasi ya Tabora.

Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Mhe. Paul Chacha (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa walimu, Prof. Masoud Hadi Muruke (kulia) na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (kushoto) mara baada ya kikao kifupi ofisini kwake tarehe 5 Juni, 2025.

Bi. Asha Lubuva Ateuliwa Mkurugenzi Msaidizi wa Maadili na Nidhamu TSC

Na Mwandishi Wetu – Dodoma.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imetangaza kumpandisha cheo na kumteua Bi. Asha Hamis Lubuva kuwa Mkurugenzi Msaidizi, Sehemu ya Maadili na Nidhamu, uteuzi ambao ulianza rasmi tarehe 20 Juni, 2025.

Taarifa hiyo imetolewa na Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu wa Tume, Bw. Zachary Dida tarehe 23 Juni 2025 kwa niaba ya Katibu wa Tume.

Taarifa hiyo iliweka bayana kuwa uteuzi huo umetolewa kwa mujibu wa mamlaka aliyopewa Katibu chini ya Kifungu cha 6(1)(b) cha Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298.

“Kwa niaba ya Katibu wa Tume, tunampongeza Bi. Asha Lubuva kwa uteuzi huu wa heshima. Ni ishara ya imani kubwa kwa uwezo wake wa kitaaluma, uadilifu, na moyo wa kujituma katika kusimamia masuala ya walimu nchini,” ilisomeka sehemu ya taarifa hiyo.

Itakumbukwa kuwa nafasi ya Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Maadili na Nidhamu ilikuwa wazi baada ya aliyekuwa akishika nafasi hiyo, Mwl. Robert Lwilele kustaafu ambapo Bi. Asha alikuwa anakaimu nafasi hiyo.

Bi. Lubuva ana uzoefu wa kutosha kwani amekumua afisa wa kawaida katika Sehemu ya Maadili na Nidhamu Tume ya Utumishi wa Walimu kwa miaka kadhaa ambapo alijikita katika masuala ya usimamizi wa maadili ya walimu ikiwa ni pamoja na uchakataji wa mashauri ya nidhamu, uchambuzi wa rufaa pamoja na utoaji elimu kwa walimu.

Tume ya Utumishi wa Walimu imemtakia mafanikio mema katika utekelezaji wa majukumu yake mapya, ikisisitiza kuwa uteuzi huo ni chachu ya maendeleo endelevu ya walimu na ustawi wa sekta ya elimu kwa ujumla.



MWL. NKWAMA ATEMBELEA BANDA LA TSC, MAADHIMISHO YA WIKI YA UTUMISHI WA UMMA



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akionyesha moja ya vitabu vilivyokuwa vinapatikana katika banda la TSC wakati wa Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma tarehe 16 June, 2025.

Na Mwandishi wetu – Dodoma.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama tarehe 16 June, 2025 ametembelea banda la TSC katika maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yanayofanyika katika viwanja vya Chinangali Park jijini Dodoma.

Akiwa katika banda hilo, Mwl. Nkwama ametoa wito kwa walimu na wadau mbalimbali kutumia fursa ya maadhimisho hayo kutembelea banda la TSC kwa lengo la kutatuliwa changamoto zao pamoja na kupata elimu ya masuala mbalimbali ya utumishi wa walimu.

Maadhimisho hayo kwa mwaka huu yamebeba kaulimbiu isemayo, “Himiza matumizi ya mifumo ya kidigitali ili kuongeza upatikanaji wa taarifa na kuchagiza uwajibikaji,” na yanatarajiwa kufunguliwa rasmi tarehe 17 Juni, 2025 na yatahitimishwa tarehe 23 Juni 2025.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akisikiliza maelezo ya watoa huduma alipotembelea banda la TSC wakati wa Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma tarehe 16 June, 2025.

MWL. NKWAMA ATEMBELEA BANDA LA TSC, MAADHIMISHO YA WIKI YA UTUMISHI WA UMMA



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akizungumza na watoa huduma alipotembelea banda la TSC wakati wa Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma tarehe 16 June, 2025.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akisini kitabu cha wageni alipotembelea banda la TSC wakati wa Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma tarehe 16 June, 2025.

TSC ITILIMA WATOA KONGOLE KWA RAIS SAMIA KWA UTATUZI WA CHANGAMOTO ZA WALIMU

Na Mwandishi Wetu – Itilima.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Itilima imeipongeza Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudi kubwa za kutatua kero za walimu nchini.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibu na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC ngazi ya Wilaya ya Itilima, Bw. Julius D. Sayi wakati wa mahojiano ya Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita.

Alisema kuwa katika kipindi cha uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan jumla ya walimu 1731 wamepandishwa vyeo ikiwa wa Shule za Msingi ni walimu 1305 na Sekondari ni walimu 426.

“Serikali hii imefanya makubwa kwani walimu waliokuwa na changamoto za madaraja asilimia kubwa wamepelekwa kwenye madaraja yao kulingana na umri kazini kitu ambacho kimeongeza ufanisi na kujituma kwa walimu katika kutekeleza majukumu,” alisema.

Bw. Sayi aliongeza kuwa Serikali imeweza kuajiri jumla ya walimu 343 kiwa wa shule za Msingi ni walimu 192 na Sekondari walimu 151.

Wakati huo huo Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Itilima imesema kuwa Mafunzo kwa Wakuu wa Shule na Wajumbe wa Kamati za Ajira, Upandishwaji vyeo na Nidhamu wa Tume ya Utumishi wa Walimu ngazi Wilaya yamewasaidia kuhakikisha walimu wanatekelezaji wajibu wao kwa weledi na uadilifu.

Bw. Sayi alisema kuwa kupitia mafunzo hayo, Wajumbe wa Kamati za Wilaya yamesaidia kuleta matokeo chanya katika kushughulikia mashauri ya kinidhamu kwa walimu ambapo wajumbe wameweza kutambua kasoro zilizokuwa zinajitokeza katika mchakato mzima wa uchakataji wa shauri ya nidhamu ya walimu.

Aliongeza kuwa mafunzo kwa Wakuu wa Shule yamesaidia kujua wajibu wao na kutambua kuwa wao ndiyo wanawafahamu walimu walionao vituoni kwa kujua tabia ya kila Mwalimu kumsaidia ili kuepuka kuingia kwenye makosa ya kinidhamu.

Bw. Sayi alisema kuwa mafunzo yamewasaidia kutambua adhabu na makosa pale wanapokuwa wanataka kutoa uamuzi.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Itilima, Bw. Julius Sayi (kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na Afisa wa Tume katika Ofisi hiyo, Bw. Hidelfphonce M. Celestine (kulia).



Kaimu Katibu Msaidizi TSC Wilaya ya Itilima, Bw. Julius Sayi (kushoto) akiwa anaonesha zawadi ya kalenda aliyopewa kutoka ofisi ya TAKUKURU baada ya kumaliza mafunzo ya kupambana na Rushwa na UKIMWI mahala pa kazi yaliyofanyika tarehe 13 Februari, 2025 ofisini kwake. Kulia ni Afisa maadili, Bw. Hidelfphonce Celestine.

TUME YA UTUMISHI WA WALIMU KUTOA UAMUZI WA RUFAA ZA WALIMU 44

Na Mwandishi Wetu – Morogoro.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imefanikiwa kuamua Rufaa 44 za walimu waliokata kupinga maamuzi ya mamlaka ya nidhamu ya TSC ngazi ya Wilaya zilizotoa adhabu dhidi yao.

Takwimu hizo zimetolewa tarehe hivi karibuni na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama katika Mkutano Maalum 2/2024/2025 wa Tume uliofanyika kwa siku tano, tarehe 23 – 27, Juni 2025 mkoani Morogoro.

Alisema kuwa katika maamuzi yaliyotolewa, rufaa 17 zilirudishwa kwa ajili ya kuanzishwa upya baada ya kuonekana mwenendo wa uendeshaji wa mashauri uliokuwa na dosari huku rufaa 11 zilikataliwa na adhabu zilizotolewa na Mamlaka za Nidhami zilizidhibitishwa.

Mwl. Paulina aliongeza kuwa Tume hiyo ilizikubali rufaa 10 na adhabu ziliyotolewa zilizotolewa na



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke akizungumza wakati wa mkutano maalumu wa siku tano wa Tume ya Utumishi wa Walimu mjini Morogoro hivi karibuni.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akitoa majumusiho ya rufaa zilizoamuliwa katika mkutano wa Tume maalumu uliofanyika mjini Morogoro hivi karibuni.

Mamlaka za Nidhamu zilitenguliwa.

Aliendelea kueleza kuwa Rufaa 6 hazikusikilizwa baada ya kubainika kuwa warufani waliwasilisha rufaa zao nje ya muda wa siku 45 tangu tarehe ya kupokea uamuzi wa shauri ikiwa ni matakwa ya Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura ya 448 na Kanuni zake za mwaka 2016.

Pamoja na kutoa maamuzi hayo, Wajumbe wa Tume walitoa elimu pamoja na ushauri kwa walimu waliofika mbele ya Tume ya Utumishi wa Walimu kujitetea, ili kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Tume ya Utumishi wa Walimu ili kutokiuka maadili ya kazi wakati wa utekelezaji wa majukumu yao.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Masoud Hadi Muruke aliwashukuru Wajumbe na Seketrarieti ya Tume kwa kufanikisha mkutano huo.

Katika Mkutano huo jumla ya walimu tisa kati ya 44 walifika mbele ya Tume kwa ajili ya kutoa utetezi wao na kuomba adhabu dhidi yao zitenguliwe.

TUME YA UTUMISHI WA WALIMU KUTOA UAMUZI WA RUFAA ZA WALIMU 44



Baadhi ya Wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakiwa katika mkutano maalumu wa Tume ya Utumishi wa Walimu uliofanyika hivi karibuni mjini Morogoro.



Baadhi ya Washiriki wa Mkutano Maalumu wa Tume uliofanyika hivi karibuni mjini Morogoro wakiwa kwenye Mkutano huo.

MAFUNZO KWA MAMLAKA ZA NIDHAMU YAONGEZA UFANISI KATIKA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU-TSC KAHAMA

Na Mwandishi Wetu- KAHAMA

Mafunzo kwa Wakuu wa Shule na Wajumbe wa Kamati za Ajira, Upandishwaji Vyeo na Nidhamu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ngazi Wilaya yamewasaidia kuhakikisha walimu wanatekelezaji wajibu wao kwa weledi na uadilifu.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kahama, Bw. Marco Badehe Emmanuel wakati wa mahijiano na Maafisa wa TSC Makao Makuu kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita.

Alisema kuwa mafunzo hayo yameleta matokeo chanya katika kushughulikia mashauri ya kinidhamu kwa walimu na kuwajengea Wajumbe uwezo wa kutambua makosa na adhabu zake hivyo kutoa adhabu zinazoendana na makosa yaliyotendwa.

Katika hatua nyingine TSC Wilaya ya Kahama imeishukuru Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Rais, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa utatuzi wa kero na changamoto zilizokuwa zikiwakabili walimu nchini.

Bw. Emmanuel alisema kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imeajiri idadi kubwa ya walimu wa Shule ya Msingi na Sekondari na kutolewa kwa vibali vya kupandishwa vyeo ambavyo hapo awali vilisitishwa.

Alisema kuwa katika uongozi wa Rais Samia jumla ya walimu 3,127 wamepandishwa vyeo ikiwa wa Shule za Msingi ni 2,240 na Sekondari ni 887 katika Wilaya ya Kahama.

Aidha, Bw. Emmanuel alisema kuwa Wilaya hiyo imepokea jumla ya walimu wa ajira mpya 217 ambapo wa Shule za Msingi ni 206 na walimu tisa (9) ni wa Shule za Sekondari.

Wakati huo huo, Bw. Emmanuel alisema kuwa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kahama imeongeza nguvu katika ziara za utoaji elimu kwa




Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kahama, Bw. Marco Badehe Emmanuel akiendelea na majukumu majukumu yake ya kazi.

walimu ili kuhakikisha kuwa walimu wengi hawaingii katika mashauri ya kinidhamu.

Bw. Emmanuel alisema kuwa Tume ya Utumishi Walimu Wilaya ya Kahama kwa kushirikiana na

Wakuu wa shule na Maafisa Elimu Kata wamekuwa wakifanya ziara za pamoja kwa ajili ya kutatua changamoto za walimu pamoja na kutoa ushauri wa masuala mbalimbali ya kiutumishi.

KILOLO YANEEMEKA NA UONGOZI WA RAIS SAMIA: Walimu 1,062 Wapandishwa Vyeo Ndani ya Miaka Miwili.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kilolo Bw. Laiton Ng'amilo akiwa ofisini akitekeleza majukumu yake.



Maafisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ngazi ya Wilaya ya Kilolo

Na Mwandishi Wetu, Kilolo

Walimu zaidi ya 1,000 katika Wilaya ya Kilolo mkoani Iringa wamepandishwa vyeo ndani ya kipindi cha miaka miwili ikiwa ni matunda ya uongozi bora wa Serikali ya Awamu ya Sita, hatua inayotajwa kuleta faraja kubwa na hamasa kwa walimu wilayani humo.

Taarifa hiyo imetolewa na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kilolo, Bw. Laiton Ng'amilo, wakati wa mahojiano maalum na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

wa TSC hivi karibuni.

"Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024 na 2024/2025, walimu 1,062 wa shule za Serikali wamepandishwa vyeo. Kati yao, 668 ni walimu wa shule za msingi na 394 ni wa sekondari," alisema Bw. Ng'amilo huku akionesha furaha kwa niaba ya walimu wa wilaya hiyo.

Kwa mujibu wa Ng'amilo, mafanikio hayo ni matokeo ya dhamira ya dhati ya Rais Samia kutatua changamoto za walimu kwa vitendo, ikiwemo kushughulikia kwa wakati stahiki za upandishwaji wa vyeo, kubadilisha miundo ya kazi, pamoja na ajira mpya zinazotolewa kila mwaka.

"Ofisi ya TSC Kilolo ina mengi ya kujivunia chini ya Awamu ya Sita. Malalamiko ya walimu yanapokelewa na kufanyiwa kazi kwa kasi isiyowahi kushuhudiwa," alisema kwa msisitizo.

Aidha, alibainisha kuwa kupitia Kliniki ya Mama Samia, walimu wamekuwa na jukwaa la moja kwa moja kuwasilisha malalamiko yao na kupatiwa majibu papo hapo. "Ni mfumo wa kipekee unaobeba sura ya usikivu wa Serikali kwa watumishi wake," aliongeza.

Mbali na upandishwaji wa vyeo, Serikali pia imepiga hatua katika kulipa kwa wakati madai ya likizo kwa walimu, jambo lililokuwa kero ya muda mrefu.

WAJUMBE WA KAMATI ZA WILAYA ZA TUME WATAKIWA KUTOEGEMEA UPANDE WAKATI WA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YAO



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama akitoa maelezo ya utangulizi mjini Tabora wakati wa ufunguzi wa mafunzo Wajumbe wa Kamati za Ajira, upandishwaji vyeo na nidhamu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ngazi za Wilaya.

Na Mwandishi Wetu – Tabora.

Wajumbe wa Kamati za Ajira, Upandishwaji Vyeo na Nidhamu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ngazi za Wilaya wametakiwa kutoegemea upande wowote wanapotekeleza majukumu yao ya utoaji wa haki kwa walimu.

Kauli hiyo imetolewa tarehe 03 Juni, 2025 na Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Elimu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Dkt. Emmanuel Shindika katika hotuba aliyosoma kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa wakati wa ufunguzi wa mafunzo kwa wajumbe hao.

“Baadhi yenu ni sehemu ya waajiri, na pia ni wajumbe wa Kamati zinazohusika kutoa uamuzi kuhusu walimu, wakati mwingine kama binadamu mnaweza kushawishika kuzishawishi Kamati kwenye maamuzi yake kutekeleza kwa kuzingatia yale tunayoyafahamu. Niwasihi inapofika wakati wa kufanya maamuzi, mzingatie Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo ili kuepuka

kuegemea upande mmoja ili kuepuka ukandamizaji wa Mwalimu anapokuwa na mashauri,” alisema.

Aliwataka kufanya kazi kwa bidii, uaminifu na kwa kushirikiana na wajumbe wengine ili kuhakikisha kuwa dhamira ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuhudumia walimu na hatimaye kuinua Elimu nchii inatimia.

Aidha, Dkt. Shindika aliipongeza Tume ya Utumishi wa Walimu, kwa kuandaa na kuendesha Mafunzo hayo ambayo tayari yameshafanyika kwa asilimia 100 kwa watumishi wote wa Tume, na sasa yakifanyika kwa wajumbe wa kamati.

Aliwataka Wajumbe hao kutumia mafunzo kama nyenzo muhimu katika kutekeleza majukumu yao hususan kwenye ushughulikiaji wa mashauri ya nidhamu kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo ili kutenda haki.

“Napenda kutumia nafasi hii kuwakumbusha kuwa, jukumu la usimamizi wa masuala mbalimbali yanayowahusu walimuni jukumu letu sote kuanzia jamii, walimu, viongozi katika Shule, Kata, na Wilaya. Upande mmoja usipotekeleza jukumu lake vema, upande mwingine hautaweza kufanya kazi kwa ufanisi,” alisisitiza Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi

wa Walimu, Prof. Masoud Hadi Muruke aliwataka Wajumbe kutumia mafunzo hayo kutoa elimu kwa walimu kuhusu utumishi wao na uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu ili wasiingie katika kutenda makosa ya kinidhamu.

Alisema kuwa baada ya mafunzo anatarajia hakutakuwa na ukiukwaji wala ucheleweshwaji katika kushughulikia mashauri ya nidhamu na haki itatendeka na itaonekana kweli imetendeka kwa maamuzi yanayotolewa kwa walimu.

Prof. Muruke aliwasisitiza washiriki kuhakikisha wanakuwa makini kwa yale yote watakayofundishwa ili hatimaye wakatekeleze majukumu yao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama alisema kuwa mafunzo hayo ya siku tatu yanawashirikisha Wajumbe wa Kamati za Tume wilaya 139 kwa lengo la kuwajengea uwezo ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa uadilifu na weledi.

Alisema kuwa mafunzo hayo yatakuwa ni nyenzo muhimu ya kuondoa changamoto zilizopo na kuimarisha nidhamu na utendaji kazi katika kada ya uwalimu.

Mwl. Paulina alisema kuwa baada ya mafunzo hayo washiriki watakuwa na uwezo wa kusimamia na kuboresha uendeshaji wa mashauri ya nidhamu kwa walimu wanaowahudumia katika Utumishi wa Umma kwa haki, uwazi, usawa na ufanisi, hatimaye kuepusha ucheleweshaji wa haki na kuwa na watumishi wa umma wenye maadili na tija.

Aidha, alisema kuwa washiriki watapata nyenzo ya kutatua changamoto zilizopo katika usimamizi wa mashauri ya nidhamu na rufaa za walimu na hivyo, kuboresha mazingira ya kazi, kuimarisha utoaji wa huduma ya elimu na kukuza maendeleo ya Taifa kupitia ubora wa elimu itolewayo nchini.

Katika hatua nyingine Katibu huyo wa Tume alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa utekelezaji wa mambo makubwa kwa walimu ambapo walimu 386,479 wamepandishwa vyeo na kubadilishiwa Kada.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Masoud Hadi Muruke akitoa salamu za Tume mjini Tabora wakati wa ufunguzi wa mafunzo Wajumbe wa Kamati za Ajira, upandishwaji vyeo na nidhamu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ngazi za Wilaya.



Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Elimu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Dkt. Emmanuel Shindika akitoa hotuba mjini Tabora wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya Wajumbe wa Kamati za Ajira, upandishwaji vyeo na nidhamu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ngazi za Wilaya.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama (kushoto) na Mkurugenzi wa Idara ya Elimu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Dkt. Emmanuel Shindika (wa tatu kutoka kushoto), Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Masoud Hadi Muruke (wa pili kutoka kushoto), Meneja wa Chuo cha Utumishi wa Umma Kampasi ya Tabora, Dkt. Joseph S. Mbwiilo (kulia) na Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu Mwl. Fatuma Muya wakimkumbuka Mjumbe wa Kamati za Ajira, Upandishwaji Vyeo na Nidhamu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Mpanda, Bw. Gerald Kifyasi na mtumishi wa Tume Wilaya ya Arumeru, Mwl. Allen Simon Mduda waliofariki dunia hivi karibuni.



Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Elimu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Dkt. Emmanuel Shindika (katikati), Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Masoud Hadi Muruke (wa pili kutoka kushoto), Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kutoka kulia), Meneja wa Chuo cha Utumishi wa Umma Kampasi ya Tabora, Dkt. Joseph S. Mbwilo (kulia) na Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu, Mwl. Fatuma Muya (kushoto) wakiimba wimbo wa Taifa kabla ya ufunguzi wa mafunzo ya Wajumbe wa Kamati za Ajira, upandishwaji vyeo na nidhamu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ngazi za Wilaya tarehe 3 Juni, 2025.



Baadhi ya Viongozi kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu Makao Makuu Dodoma wakiwa na washiriki wa ufunguzi wa mafunzo Wajumbe wa Kamati za Ajira, upandishwaji vyeo na nidhamu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ngazi za Wilaya.



Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Elimu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Dkt. Emmanuel Shindika (kushoto) akisalimiana na Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Masoud Hadi Muruke (kulia) mara baada ya kuwasili katika eneo la Chuo cha Utumishi wa Umma Kampasi ya Tabora kwa ufunguzi wa mafunzo Wajumbe wa Kamati za Ajira, upandishwaji vyeo na nidhamu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ngazi za Wilaya. Katikati ni Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama.



Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Elimu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Dkt. Emmanuel Shindika (kulia) akisaini Kitabu cha Wageni katika Chuo cha Utumishi wa Walimu Kampasi ya Tabora baada ya kuwasili kwa ajili ya ufunguzi wa mafunzo Wajumbe wa Kamati za Ajira, Upandishwaji Vyeo na Nidhamu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ngazi za Wilaya. Wengine katika picha ni Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Masoud Hadi Muruke (wa pili kushoto), Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama (kushoto) na Meneja wa Chuo cha Utumishi wa Umma Kampasi ya Tabora, Dkt. Joseph S. Mbwilo (wa pili kulia).

TSC MASWA WATOA KONGOLE KWA RAIS SAMIA KWA UTATUZI WA CHANGAMOTO ZA WALIMU

**Na Mwandishi Wetu –
Maswa.**

Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Maswa inapongeza Uongozi wa Awamu ya Sita chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuondoa kero na changamoto kwa walimu nchini.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Maswa, Bw. Amon M. Nhindilo wakati wa mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa Tume ya Utumishi wa Walimu.

Alisema kuwa uongozi wa Awamu ya Sita umewapandisha vyeo jumla ya walimu 2,632 ikiwa wa Shule za Msingi ni 1,778 na Sekondari ni 854 na amebadilisha kuwa walimu 119 wakiwemo wa Shule za Msingi 89 na Sekondari 31 wamebadilishiwa vyeo baada ya kukidhi vigezo.

Bw. Nhindilo alisema kuwa Serikali imejenga miundombinu ambayo

imerahisisha ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi na walimu kwa ujumla na imeendelea kuboresha maslahi ya walimu na kuwafanya waendeleo kufanya kazi kwa utulivu.

Alisema kuwa hivi sasa walimu wa Halmashauri ya Maswa wanalipwa likizo zao na madeni mengine yanaendelea kulipwa na Serikali.

Bw. Nhindilo aliongeza kuwa jumla ya walimu 152 walisajiliwa kwa mwaka fedha 2023/2024 ikiwa wa Shule za Msingi walimu ni 104 na Sekondari walimu 46.

Alisema kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Maswa imepokea walimu 125 na walimu waliothibitishwa kazini ni 46 kwa Shule za Sekondari na walimu 102 kwa Shule za Msingi.

Katika hatua nyingine Bw. Nhindilo alisema kuwa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Maswa kwa kushirikiana na wadau kama vile Chama cha Walimu Tanzania (CWT) wamekuwa wakitembelea Shule kuongea na walimu

kuwaelimisha namna ya kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma wanapotekeleza majukumu yao.

Alisema kuwa hatua hiyo inalenga kutoa elimu kwa Walimu ili wasiingie kwenye makosa ambayo yatahatarisha utumishi wao.

Aidha, Bw. Nhindilo alisema kuwa mafunzo kwa wajumbe wa Kamati ya Wilaya yamewasaidia kutembelea Walimu na kutoa elimu ili kuwasaidia kutambua Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma wanapotekeleza majukumu yao.

Aliongeza kuwa mafunzo ya Walimu Wakuu yamesaidia kuwaongezea weledi kwenye usimamizi wa walimu katika masuala ya kinidhamu na hivyo kupunguza mashauri ya kinidhamu.

Halmashauri ya Wilaya ya Maswa ina Shule za Msingi 135 na Shule za Sekondari 47 ambao wanahudumia jumla ya walimu 631 kwa Shule za Sekondari na 1,236 kwa Shule za Msingi.

Picha za Matukio mbalimbali wakati wa Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika tarehe 16 – 23 Juni, 2025 katika viwanja vya Chinangali Park jijini Dodoma.



Picha za Matukio mbalimbali wakati wa Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika tarehe 16 – 23 Juni, 2025 katika viwanja vya Chinangali Park jijini Dodoma.



MAFUNZO KWA MAMLAKA ZA NIDHAMU ZA TSC WILAYA YA BUSEGA YAONGEZA UFANISI WA UTENDAJI KAZI

Na Mwandishi Wetu – Busega.

Mafunzo kwa Wakuu wa Shule na Wajumbe wa Kamati za Ajira, Upandishwaji vyeo na Nidhamu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ngazi Wilaya yamewasaidia kuhakikisha walimu wanatekelezaji wajibu wao kwa weledi na uadilifu.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Busega Bw. Sylvester Itoba wakati wa mahijiano na Maafisa wa TSC Makao Makuu kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita.

Alisema kuwa mafunzo hayo yameleta matokeo chanya katika kushughulikia mashauri ya kinidhamu kwa walimu na kuwajengea Wajumbe uwezo wa kutambua makosa na adhabu zake hivyo kutoa adhabu zinazoendana na makosa yaliyotendwa.

Katika hatua nyingine Tume ya Utumishi wa Walimu ngazi ya Wilaya ya Busega imeishukuru Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa utatuzi wa keroa na changamoto zilizokuwa zikiwakabili walimu nchini.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Busega, Bw. Sylvester Itoba.

Bw. Itoba alisema kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imeajiri idadi kubwa ya walimu wa Shule ya Msingi na Sekondari na kutolewa kwa vibali vya kupandishwa vyeo na nyongeza za mishahara ambavyo hapo awali vilistishwa.

“Katika uongozi wa Rais Samia jumla ya walimu 1847 wamepandishwa vyeo ikiwa wa Shule za Msingi ni 1306 na Sekondari ni 541,” alisema.

Aidha, Bw. Itoba alisema kuwa Wilaya imepokea walimu wa ajira mpya 30 wa Shule za Msingi na 63 wa Sekondari.

Wakati huo huo, Bw. Itoba alisema kuwa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Busega imeongeza nguvu katika ziara za utoaji elimu kwa walimu ili kuhakikisha kuwa walimu wengi hawaingii katika mashauri ya kinidhamu.

Alisema kuwa hatua hiyo imesaidia kupunguza mashauri ya nidhamu kwa mwaka 2023/24 Wilayani humo.

“Katika kipindi cha mwaka 2023/2024 ni shauri moja tu la kinidhamu la mwalimu wa Idara ya Elimu Sekondari lililofunguliwa ambapo hapakuwa na Shauri lolote upande wa Elimu Msingi,” alisema.

Bw. Itoba alisema kuwa Tume ya Utumishi Walimu Wilaya ya Busega kwa kushirikiana na Wakuu wa shule na Maafisa Elimu Kata wamekuwa ziara ya pamoja kwa ajili ya kutatua changamoto za walimu kwa kusikiliza na kusahihisha kabla ya kuchukua hatua yoyote.

Aliongeza kuwa wamekuwa na vikao vya walimu kwa kila Kata ambapo ofisi ya TSC hualikwa kwa ajili ya kutoa elimu na kuhudhuria vikao vya kikanda ambavyo husaidia kutoa elimu kwa walimu wote.



Afisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Bw. Lazaro Shija Samson.

TSC KISHAPU WAMSHUKURU RAIS SAMIA KWA UTATUZI WA CHANGAMOTO ZA WALIMU

Na Mwandishi Wetu – Kishapu.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kishapu imeipongeza Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudi kubwa za kutatua kero za walimu nchini.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibu na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Kishapu, Bw. Paul Amos Sheka wakati wa mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita.

Alisema kuwa katika kipindi cha uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan walimu 1,201 wamepandishwa vyeo ikiwa kwa Shule za Msingi ni walimu 738 na Sekondari ni walimu 463

“Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kishapu inajivunia uongozi wa awamu ya sita kwa kuondoa kero za walimu ikiwemo kupandishwa vyeo, kubadilishiwa vyeo/kazi kwa waliojiendeleza kielimu, kulipwa fedha za likizo kwa wakati mara fedha inapoletwa na malimbikizo ya mishahara ya nyuma kulipwa na Serikali ya awamu ya sita,” alisema.

Bw. Sheka aliongeza kuwa Serikali imeweza kuajiri jumla ya walimu 274 kwa shule za Msingi ni walimu 170 na Sekondari walimu 104.

Wakati huo huo Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kishapu imesema kuwa Mafunzo kwa Wakuu wa Shule na Wajumbe wa Kamati za Ajira, Upandishwaji vyeo na Nidhamu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ngazi Wilaya yamewasaidia kuhakikisha walimu wanatekelezaji wajibu wao kwa weledi na uadilifu.

Bw. Sheka alisema kupitia mafunzo hayo yamesaidia kuleta matokeo chanya katika kushughulikia mashauri ya kinidhamu kwa walimu ambapo wajumbe wameweza kutambua kasoro zilizokuwa zinajitokeza katika mchakato wa shauri.

Aliongeza kuwa mafunzo kwa Wakuu wa Shule yamesaidia kujua wajibu wao na kutambua kuwa



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kishapu, Bw. Amos Sheka.

wao ndiyo wanawafahamu walimu walionao vituoni kwa kujua tabia ya kila Mwalimu na hivyo kuwasiadika kuepuka kuingia kwenye makosa ya kinidhamu kama vile utoro.

Bw. Sheka alisema kuwa mafunzo

yamewasidia kutambua adhabu na makosa pale wanapokuwa wanataka kutoa uamuzi.

Alisema kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kulipa madeni ya walimu katika Wilaya hiyo.

ZIARA ZA TSC MEATU ZAZAA MATUNDA, WALIMU WAJENGEWA UELEWA KUEPUKA KUKIUKA MAADILI

Na Mwandishi Wetu, Meatu

Katika juhudi za kuimarisha maadili ya utumishi na kuondoa malalamiko ya walimu, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Meatu imeongeza kasi ya kufanya ziara za elimu kwa walimu, hatua iliyosaidia kupunguza kwa kiasi kikubwa idadi ya mashauri ya kinidhamu wilayani humo.

Kwa mujibu wa Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Meatu, Bw. Njile Ipando, tangu kuanza kwa mwaka wa fedha 2023/24, Tume hiyo kwa kushirikiana na wadau wa elimu imekuwa ikifika shuleni kusikiliza changamoto za walimu na kutoa elimu ya sheria, kanuni na miongozo ya utumishi.

"Tuliamua kupeleka elimu kabla ya kuchukua hatua za kinidhamu. Tumekuwa tukikutana na walimu kwenye vikao vya Kata, na mara nyingine tunatembelea shule moja kwa moja. Hii imepunguza sana malalamiko, lakini zaidi imejenga uelewa wa walimu juu ya haki, wajibu na namna ya kuepuka makosa ya kinidhamu," alisema Bw. Ipando wakati wa mahojiano maalum na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini



Bw. Njile Ipando, Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Meatu, akiwa kazini.

cha Tume.

Katika mwaka 2023 pekee, TSC Meatu ilifanikiwa kutoa elimu katika maeneo nane maalum yaliyotambuliwa kuwa na changamoto kubwa. Kupitia kazi hiyo, walimu wameelewa vyema kanuni za utumishi wa umma, na wameanza kujitathmini kabla ya kufanya maamuzi yanayoweza

kuwaletea matatizo kazini.

Aidha, Bw. Ipando alieleza kuwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan imekuwa nguzo kubwa ya mafanikio hayo. "Kupitia Serikali hii tumeajiri walimu 289 mwaka huu pekee, na kati yao 161 ni wa shule za sekondari na 128 wa msingi," alieleza.

Mbali na ajira, TSC Meatu pia imewathibitisha kazini walimu 264, huku 1,258 wakipandishwa vyeo – hatua ambazo zimeleta morali kubwa miongoni mwa walimu wa Wilaya hiyo. "Kwa miaka mingi walimu walikuwa wakisubiri kwa muda mrefu kuthibitishwa au kupandishwa vyeo, lakini sasa hakuna mwalimu mwenye sifa anayecheleweshwa kupanda, hii ni hatua kubwa," aliongeza.

Ofisi ya TSC Meatu inaendelea pia na mafunzo ya mara kwa mara kwa Wajumbe wa Kamati za Wilaya wanaoshughulikia masuala ya kinidhamu, ili kuhakikisha maamuzi yanayotolewa yanazingatia sheria na taratibu zote za kiutumishi.

Kwa sasa, Tume hiyo inahudumia jumla ya walimu 1,458 katika shule 159 za Serikali wilayani Meatu, ikiwa ni sehemu ya dhamira ya kitaifa ya kuboresha mazingira ya kazi, ustawi wa walimu na hatimaye kuinua ufaulu wa wanafunzi.



Bw. Josephat Msonge, Afisa Ajira na Maendeleo ya Walimu, akiendelea na majukumu katika ofisi za TSC Wilaya ya Meatu.



MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu